# BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA

## MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU

## KIDATO CHA SITA

## KISWAHILI 1

**(Kwa Watahiniwa walioko na wasiokuwa shuleni)**

**121/1**

**MUDA: Saa 3:00** **Jumanne, 3 Machi 2026 asubuhi**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali nane (8.
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali matatu (3) kutoka sehemu B. Swali **la nane (8)** ni la lazima.
3. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
5. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Shulelibrary.com

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata.

Methali hii "Mkataa pema pabaya panamwita", ni muhimu sana kuwaeleza vijana wetu kwa mustakabali chanya wa maendeleo ya nchi yetu. Hivi karibuni kumeibuka wimbi la maandamano ya kile wanachokiita ni kudai haki kwa vijana wa Kiafrika almaarufu GEN-Z.

Maandamano haya huchochewa Zaidi na mataifa makubwa yenye uchu wa rasilimali zetu tulizotunukiwa na Mwenyezi Mungu. Hufanya hivi kupitia vyombo vyao vya habari kwa **k**ueneza propaganda za hapa na pale ili kupandikiza chuki miongoni mwa wananchi na serikali zao. Pia wakati mwingine huenda mbali zaidi kwa kuwalipa pesa wahaini na wasaliti wa nchi zao chini ya mwamvuli wa uanaharakati ili kuhakikisha dhamira zao zinakamilika ipasavyo.

La haula! Amakweli "Vita vya panzi furaha ya kunguru", wakifanikiwa kutuingiza kwenye mtego wao. Wanakuja kujichotea na kusaza rasilimali zetu kwa mwamvuli wa Kulinda amani kama tuonavyo kwa baadhi ya mataifa yaliyouingia mkenge huu, kama vile Libya, Sudan na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Rai yangu ni kuwataka wazazi na jamii kwa ujumla kutahadharishana kuhusu jambo hili, maana athari zake ni kubwa na zisizoweza kutaturika kirahisi kama tunavyodhania. Tujitahidi kuilinda hii tunu ya amani tuliyoirithi kutoka kwa mababu zetu nasi tuwarithishe wanetu na wajukuu zetu. Niwaache na ule usemi usemao "Ukitaka kuona umuhimu wa makalio kalia kichwa".

**MASWALI:**

(a) Pendekeza kichwa cha habari uliyosoma.

(b) Fafanua mbinu mbili (2) zinazotumiwa na mataifa makubwa kueneza propaganda kwenye mataifa yanayoendelea kiuchumi.

(c) Eleza maana za methali zilizotumiwa na mataifa makubwa kueneza propaganda zao kwenye mataifa yanayoendelea kiuchumi.

(d) Je, unadhani ni athari gani zinazoweza kuletwa na janga linaloelezwa na mwandishi wa habari hapo juu? Toa hoja mbili (2).

(e) Ukiwa kama mwanadiplomasia, unadhani nini kifanyike ili kuzinusuru nchi za Kiafrika na janga hili? Toa hoja mbili (2).

Shulelibrary.com

2. Baada ya kumaliza mada ya Ngeli za Nomino, Mwalimu Majuto aliwapa kazi wanafunzi wa kidato cha sita kufafanua aina tano (5) za upatanisho wa kisarufi. Ukiwa miongoni mwa wanafunzi mahiri darasani, onesha namna unavyoweza jukumu hilo kwa mifano.

3. "Mama anaupiga mwingi" ni miongoni mwa kauli zilizotamalaki sana miongoni mwa Watanzania na hata nje ya mipaka ya Tanzania. Tumia maarifa uliyoyapata darasani kueleza njia zinazosababisha kuibuka kwa maneno kama haya katika jamii yako. Toa hoja tano (5) tu na mifano.

4. (a) Umeteuliwa kushiriki katika kongamano la Kiswahili linalohusisha wanafunzi wa sekondari hapa nchini. Jukumu lako katika kongamano hili ni kubainisha tofauti za kimuundo zilizopo kati ya sentensi ambatani na sentensi changamani. Tumia aya moja tu yenye mashiko katika ufafanuzi wako.
   (b) Kama mmoja wa wahamasishaji wa matumizi ya lugha fasaha shuleni kwako, wasaidie wanafunzi wenzako kuweka wazi mazingira yanayopelekea kutokea kwa vielezi katika lugha ya Kiswahili, kisha taja aina ya kielezi kwa kila muktadha kwa msaada wa sentensi. Toa hoja nne (4) tu.

Shulelibrary.com

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **matatu (3)** kutoka sehemu hii. Swali la **nane (8)** ni la lazima.

5. Kashinde ni mshindi wa jumla katika shindano la uandishi wa Risala nchini Tanzania kwa mwaka wa masomo 2025 – 2026; wanafunzi wengi wa kidato cha sita wanatamani kujua siri ya mafanikio mbali na kumpongeza. Ukiwa rafiki wa karibu wa Kashinde, wabainishie mambo sita (6) aliyozingatia na kuchagiza ushindi wake.

6. Mara baada ya kujipatia uhuru mwaka 1961, serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilifanya juhudi kubwa katika kukuza na kueneza lugha adhimu ya Kiswahili kupitia sekta ya elimu. Ukiwa kama mzalendo wa Taifa hili, thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutoa hoja sita (6) na mifano.

7. Wanaharakati wengi wa lugha ya Kiswahili bado wanapinga Marekani kuwa Makao Makuu ya Chama cha ukuzaji wa Kiswahili duniani (CHAUKIDU) kutokana na historia ya Kiswahili, lakini bado chama hiki kina nguvu katika utekelezaji wa majukumu yake barabara. Ukiwa kamka mlumbi wa Kiswahili, eleza majukumu sita (6) yanayotekelezwa na chama hicho bila ya kuingiliwa na taifa lolote.

8. "Hakuna kazi ya tafsiri inayoweza kukamilika bila ya kuwepo kwa udurusu wa rasimu ya kwanza," kwa kutumia maarifa uliyoyapata darasani dadavua faida za kutekeleza jukumu hilo kwa wataalamu wa tafsiri na ukalimani. Toa hoja tano (5) na mifano.

*Wabillah Tawfiiq*

Shulelibrary.com